

Viongozi wa dini wakumbushwa wajibu

Mtumwa Ally na
Joyce Ngwembele

■■Viongozi wa dini nchini wametakiwa kujiepusha na mambo ambayo yataapelekea uvunjifu wa amani katika kipindi cha uchaguzi na baada ili kuiweka nchi katika hali ya usalama.

Hayo yameelezwa jana jijini Dar es Salaam na Shekhe Mkuu wa Dar es Salaam, Mussa Salum wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema kuwa, viongozi hao ndio wenyewe nguvu kubwa katika kuleta amani nchini na hivyo kuwataka kuwahimiza watu katika kudumisha kuwepo kwa amani ndani ya nchi.

"Tunaamini kuwa viongozi kwa kutumia nyadhifa zao wana mchango mkubwa katika kuleta amani ya nchi kwa kipindi hiki kinachokuja cha uchaguzi kwa kutunza amani iliyopo kwa sasa," alisema Mussa.

Kwa upande wake Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Ernest Mangu alisema Jeshi

la Polisi wamejipanga vizuri kwa kuwapa elimu askari wao pamoja na wananchi juu ya umuhimu wa uchaguzi.

"Sisi kama Jeshi la Polisi tumejipanga vizuri ili kukabiliana na hali ya kuendeleza amani iliyopo pamoja na kuendeleza kanuni na sheria za uchaguzi," alisema IGP Mangu.

Hata hivyo alisema kuwa, endapo mtu atashindwa kutii sheria basi hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake na kuonekana kama amevunja amani iliyopo kwa sasa.

Naye Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa, Alvaro Rodriguez alisema kuwa watachangia katika kusimamia uchaguzi ili isiwe chanzo cha vurugu zitakazotokea kwa kipindi chote cha uchaguzi.

"Sisi kama Umoja wa Mataifa tumejipanga kusimamia uchaguzi ufanyike kwa amani na utulivu... hali ya amani ikivunjika ni ngumu kuirudisha," alisema Alvaro.